



Nataka kujilinda na kulinda watu walio karibu nami kutokana na magonjwa.




Chanjo ni dawa ambayo hulinda watu kutokana na magonjwa.



Wakati mwingine unahitaji chanjo moja tu kwa mwaka, wakati mwingine unahitaji zaidi kulingana na chanjo.




Ninaweza kupata chanjo kutoka kwa duka lolote la dawa, daktari au kliniki yoyote.



Nitaingia kwenye jengo na kujiandikisha kwa kupeana jina langu, tarehe ya kuzaliwa, na kujibu maswali kutoka kwa msaidizi.




Familia yangu inaweza kunisaidia kujiandikisha. Msaidizi atanionyesha mahali pa kwenda. Nitaenda na msaidizi na familia yangu.



Wasaidizi wanaweza kuwa wamevaa gauni, glavu, na barakoa.




Ingawa siwezi kuona nyuso zao, wasaidizi wanafurahi sana kuniona.




Nitakunja mkono wa vazi langu au kuvua koti langu ikifika zamu yangu.




**Nitaketi kwa kiti.
Nitajaribu kutulia.**




**Muuguzi atanidunga
sindano. Ninaweza kuhisi
uchungu sindano
inapoingia kwenye mkono
wangu.**



**Muuguzi ataweka bendeji
kwenye mkono wangu.**



Familia yangu itafurahi sana kuona kuwa ninajilinda kutokana na magonjwa.



Ninaweza kuombwa nisubiri dakika 15 baada ya kupokea chanjo yangu. Ninaweza kuondoka baada ya kudungwa sindano.



Ninaweza kuendelea kujilinda mimi mwenyewe pamoja na wengine kwa kunawa mikono yangu. Ninajivunia kupata chanjo.

